
# MSANII

**TOLEO LA SABA, MACHI 2025**



**Tuzo za TMA, zatikisa nchi ukumbi wa Thesuperdome.....**

Mastaa mbalimbali wa muziki nchini wamejitokeza kwa wingi katika ukumbi wa “The Super dome” ..............

**“TRA na BASATA” zasomana kimifumo.**

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa kushirikiana na Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) wame-saini hati raasmi ya makubaliano katika ofisi kuu za TRA................





DIRA



## Dkt. Kedmon Mapana

Katibu Mtendaji
Baraza la Sanaa la Taifa
(BASATA)

Ninaamini sanaa ni nguzo muhimu katika maendeleo ya taifa letu ninawaomba wadau wa sanaa -Wasanii, Wawekezaji,Vyombo vya habari na mashirika mbalimbali tushirikiane kwa karibu  ili kuleta mabadiliko chanya, Tuwe na nidhamu, ubunifu na juhudi za pamoja kuhakikisha sanaa ya Tanzania inapata nafasi yake katika jukwaa la kimataifa



# YALIYOMO

Usiku wa Mastaa Superdome Masaki" wengi waondoka na Tuzo

Sanaa sekta mtambuka kueneza vivutio vya utalii.

Mutual generation" wapata somo la uchumi katika Sanaa

SHISAMA yaahidi kushirikiana na Mama ongea na Mwanao kuifikia Jamii

BASATA yaipongeza "Mama ongea na mwanao" kwa kuwashika mkono wenye uhitaji

Wasanii waitikia wito wa "Rais" kupima afya zao

Waziri mkuu atoa "sapoti" ya vifaa vya muziki kuinua Sanaa

TRA na BASATA" zasomana kimifumo

Magic vibe" watambua mchango wa Dkt Mapana katika sanaa

Katibu mkuu TAMISEMI ahimiza uharaka wa kuunganisha mfumo wa AMIS na TAUSI

Wajumbe wa Bodi waungana na wasanii kupima afya ya Moyo

Wajumbe wa Bodi waungana na wasanii kupima afya ya Moyo

## “Usiku wa Mastaa Superdome Masaki” wengi waondoka na Tunzo

Na. Isack N. Bilali

Mastaa mbalimbali wa muziki nchini wamejitokeza kwa wingi katika ukumbi wa “The Super dome” kushiriki katika usiku wa Tunzo za muziki Tanzania zinazoratibiwa na Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), zilizobeba ushindani mkali kati ya wasanii, huku kila kipengele kikiakisi shahuku kwa mashabiki.

Tunzo za Muziki Tanzania msimu wa 2023 umefungua njia kimataifa mara baada ya waandaaji wake kushirikiana na makampuni makubwa ya kimataifa katika tasnia ya burudani kama vile BET na MTV

Aidha, tunzo hizo zimeweza kuwapa heshima wasanii mbalimbali wakiwemo wakongwe pamoja na vipaji vipya ambavyo vinavyokuja juu katika tasnia ya muziki.

Hafla ya ugawaji tunzo, imefungwa kwa shamrashamra, huku wasanii mbalimbali wakiwapa mashabiki burudani ya moja kwa moja, wakionyesha uwezo wa kipekee walioupamba kwenye muziki wao.

1. Msanii Bora wa Muziki wa Taarab wa Mwaka
Sina Wema – Mfalme Mzee Yusuph – Mshindi
2. Wimbo Bora wa Kanda ya Mashariki, Magharibi, na Kusini mwa Afrika
Lonely At The Top – Asake – Mshindi




3. Msanii Bora wa Kiume
Shuu! – Diamond Platnumz – Mshindi
4. Msanii Bora wa Kike wa Mwaka
Falling – Nandy – Mshindi
5. Wimbo Bora wa Mwaka
Single Again – Harmonize – Mshindi
6. Mwimbaji Bora wa Muziki wa Dansi wa Mwaka
Kanivuruga – Christian Bella – Mshindi
7. Wimbo Bora wa Muziki wa Dansi wa Mwaka
Achii – Diamond Platnumz ft. Koffie Olomide – Mshindi




8. Mtunzi Bora wa Muziki wa Dansi wa Mwaka
Christian Bella – Mshindi
9. Mtunzi Bora wa Mwaka
Marioo – Mshindi
10. Mtayarishaji Bora wa Muziki wa Bongo Flava
S2Kizzy – Mshindi
11. Wimbo Bora wa Bongo Flava wa Mwaka
Mahaba – Alikiba – Mshindi
12. Mwimbaji Bora wa Kike wa Bongo Flava wa Mwaka
Naringa – Zuchu – Mshindi

13. Mwimbaji Bora wa Kiume wa Bongo Flava wa Mwaka
Mahaba – Alikiba – Mshindi
14. Msanii Bora wa Singeli wa Mwaka
Nije Ama Nisije – Dulla Makabila – Mshindi
15. Wimbo Bora wa Singeli wa Mwaka
Kitu Kizito – Rayvanny ft. Misso Misondo – Mshindi
16. DJ Bora wa Mwaka
DJ Ally B – Mshindi
17. Mwimbaji Bora wa Kike wa Mwaka
Nani Remix – Zuchu – Mshindi
18. Mwimbaji Bora wa Kiume wa Mwaka
Shu! – Diamond Platnumz – Mshindi16. DJ Bora wa Mwaka
DJ Ally B – Mshindi
17. Mwimbaji Bora wa Kike wa Mwaka
Nani Remix – Zuchu – Mshindi
18. Mwimbaji Bora wa Kiume wa Mwaka
Shu! – Diamond Platnumz – Mshindi
19. Mtayarishaji Bora wa Muziki wa Mwaka
S2Kizzy – Mshindi
20. Albamu Bora ya Mwaka
Visit Bongo – Harmonize – Mshindi
21. Msanii Chipukizi Bora wa Mwaka
Gibela – Chino Kidd – Mshindi
22. Wimbo Bora wa Hip-Hop wa Mwaka
Current Situation – Country Wizzy – Mshindi
23. Msanii Bora wa Hip-Hop wa Mwaka
Stupid – Young Lunya – Mshindi
24. Ushirikiano Bora wa Mwaka
Enjoy – Jux ft. Diamond Platnumz – Mshindi







Pamoja na yote tunzo hizo zimekonga nyoyo za wadau mbalimbali kwa namna zinavyozidi kuwa bora kila mwaka, pia limekuwa sehemu sahihi kwa wasanii kujitangaza na kupanua wigo wa kibiashara kutengeneza ushirikiano wenye nguvu na nia thabiti kuinua tasnia ya Sanaa, wengi wao wamefurahia namna serikali inavyoonesha kujali sekta ya ubunifu.





**Sanaa sekta mtambuka kueneza vivutio vya utalii.**

Na. Isack N. Bilali

Katibu Mkuu Wizara ya Habari Utamaduni, Sanaa na Michezo na Msemaji Mkuu wa Serikali Gerson Msigwa amesema Sanaa ni sekta mtambuka hivyo ushiriki wa TANAPA katika tamasha la Filamu na Sanaa umeongeza wigo kwa wasanii kujua vivutio vya utalii na maeneo ambayo vivutio hivyo vinapatikana.

"Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania linalosimamia hifadhi 21 nchini na lina maeneo mengi yenye mandhari nzuri, wanyama wengi wa aina tofauti, maua na Maporomoko ya maji yenye vina virefu na vinavyovutia ambavyo vikionekana katika "video" zenu mtaongeza wafuasi wenu na kuiuza Tanzania kimataifa," alisema Katibu Mkuu Msigwa.

Katibu Mkuu ameyasema hayo wakati wa kuhitimisha Tamasha la Kimataifa la Maendeleo ya Filamu na Sanaa nchini lililoanza tarehe 11 hadi 15 Disemba 2024 katika Viwanja vya Posta Kijitonyama jijini Dar es Salaam.

Aidha, Msigwa ameongeza, "Maelezo mliyoyapata kutoka kwa maafisa wa Sekta ya Sanaa na hawa wa uhifadhi yatakuwa yamewaongezea uelewa na yawe chachu ya kutembelea vivutio hivyo ili mujionee hazina kubwa ya maliasili tulizo nazo ili nanyi muwe katika mnyororo wa kuvitangaza kupitia kazi zenu za usanii."

Ushirikiano baina ya mashirika ya uhifadhi na sekta ya Sanaa nchini katika utekelezaji wa majukumu itakuwa ni chachu kwa wadau mbalimbali ambao Pamoja na kutembelea maeneo hayo pia wameshauriwa kufikiria namna ya kuwekeza katika hifadhi hizo, kwa kufanya hivyo watakuwa wameunga mkono jitihada za Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan za kuutangaza utalii wetu.

Kwa upande wake Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi Fredrick Malisa amesema kuwa, Shirika la hifadhi linashirikiana vizuri sana na wasanii hivyo wanawakaribisha kutembelea hifadhi hizi kwani zimejaliwa kuwa na hazina kubwa ya Maliasili.wasio watanzania kuhamasika zaidi kuzitembelea hifadhi za Taifa ili kujionea vivutio.

Juu ya hapo, Katibu Mtendaji BASATA, Dkt. Kedmon Mapana ameshukuru washiriki wote kwa namna walivyojitoa kushiriki katika Tamasha hilo ambalo limelenga kuunga mkono juhudi za serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kuitangaza nchi na kufungua diplomasia ya kiuchumi na utamaduni, hivyo ni wakati sahihi wa kuitumia Sanaa katika kutatua changamoto mbalimbali za utoaji wa huduma za kijamii, kuinua na kuonesha fursa za kiuchumi Pamoja na kuitangaza Tanzania kwa ngazi ya Kimataifa.

Wakati wote wa tamasha hilo, BASATA limejikit kutoa mafunzo kwa wasanii na wadau wa Sanaa juu ya matumizi ya mbinu za kisasa na kuifanya Sanaa kuwa biashara Pamoja na kuhimiza ulinzi wa urithi wa utamaduni wa kitanzania kwa kuzingatia maadili katika shughuli zao.

BASATA na bodi ya Filamu imeendelea kuratibu matamasha mbalimbali likiwemo Tamasha hili l Kimataifa la Maendeleo ya Filamu na Sanaa nchini na maonesho mbalimbali ya kitaifa na kimataifa ili kutangaza sekta ya Sanaa na fursa za uwekezaji ikiwemo utalii.







## “Mutual generation” wapata somo la uchumi katika Sanaa




Na Isack N. Bilali

Mkurugenzi wa Ukuzaji na Maendeleo ya Sanaa wa BASATA, Bw. Edward Buganga, amewataka viongozi wa “Mutual Generation International” (MGI) kutumia muda wao mwingi katika kuibua na kuendeleza shughuli zinazogusa sekta ya kiwanda cha ubunifu ili kupunguza changamoto ya upungufu wa ajira miongoni mwa vijana nchini.

Ameyasema hayo mara baada ya kutemebelewa na vijana wa “Mutual Generation International” katika ofisi za Baraza la Sanaa la Taifa ambapo waliweza kufanya kikao cha pamoja kujadiliana shughuli mbalimbali zinazofanywa na BASATA ambazo zina uwiano kiutendaji kwa pande zote mbili.

“Mutual Generation International” chini ya Mtendaji mkuu Elia Mwigah ni shirika lisilo la kiserikali ambalo linakukuza maendeleo ya jamii kwa kuongeza elimu ya kujitegemea, ujuzi wa kujiajiri, ufadhili wa watoto, utetezi wa mabadiliko ya hali ya hewa, udhamini wa kiufundi, kuibua na kuinua vipaji katika maendeleo ya kazi, kupanua utoaji wa huduma za kijamii, ufahamu wa sera na uchambuzi wa fursa za kidiplomasia.

Majadiliano hayo, yameshirikisha wakurugenzi wasaidizi na maafisa wa Baraza ambao kwa pamoja, wamekutana na vijana kutoka “Mutual Generation International” katika ofisi za BASATA zilizopo Kivukoni, Posta, jijini Dar es Salaam.

Ziara hiyo imelenga kuimarisha ushirikiano pamoja na kutoa elimu ya “Sanaa Biashara” kwa vijana hao ili waweze kuzifikia fursa zilizopo katika sekta ya sanaa zinazoweza kuwasaidia kujiajiri, kukuza uchumi wao, na kutatua changamoto mbalimbali

**SHISAMA yaahidi kushirikiana na Mama ongea na Mwanao kuifikia Jamii**

Na Isack N. Bilali



Raisi wa Shirikisho la Sanaa za Maonesho nchini, Bi. Cynthia Henjewele, ametangaza kuwa Shirikisho hilo litaendelea kushrikiana bega kwa bega na katika matukio yote ya kusaidia jamii yatakayoandaliwa na Taasisi ya Mama Ongea na Mwanao inayoongozwa na Msanii nguli Steve Mengele almaarufu Steve Nyerere.

Amefikia uamuzi uo baada ya Shirikisho lake kuvutiwa na shughuli mbalimbali za kusaidia jamii zinazofanywa na Taasisi hiyo jambo ambalo linagusa jamii ya watu wenye uhitaji ambao kwa asilimia kubwa wanakosa msaada hivyo kwao itakuwa wakati sahihi kutoa ushirikiano wa dhati.





Katika hatua nyingine ya kugusa moyo, Bi. Henjewele alimchangia mtoto mwenye ulemavu kiasi cha fedha ili ziweze kutumika katika kutatua baadhi ya mahitaji yake ya msingi, pia amewataka wanajamii hususani wasanii kuendelea kuwa mfano wa kuigwa katika kusaidia jamii kwakuwa hao ndo mashabiki wa kwanaza wa kazi zao za Sanaa

Taasisi ya Mama Ongea na Mwanao iliandaa hafla maalum katika ukumbi wa Karimjee jijini Dar es salaam, ambapo waliwaleta pamoja watu wenye mahitaji maalum kisha kuwapatia misaada ya mahitaji muhimu tukio hilo limefanyuika kwa kushirikiana na wadau mbalimbali limeibua mshikamano wa kijamii katika kuwajali watu wenye mahitaji maalum.

## BASATA yaipongeza “Mama ongea na mwanao” kwa kuwashika mkono wenye uhitaji

Na Isack N. Bilali

Katibu Mtendaji wa BASATA, Dkt. Kedmon Mapana, ameipongeza taasisi ya Mama Ongea na Mwanao inayoongozwa na Msanii nguli Steve Mengele almaarufu Steve Nyerere kwa kuandaa hafla maalum kwa watu wenye mahitaji maalum kisha kuwapatia mahitaji yao ya msingi jambo ambalo linakuza utu wa mwanadamu.





Ametoa pongezi hizo Katika tukio lililofanyika katika ukumbi wa Karimjee, ambapo Katibu Mtendaji BASATA, Dkt. Kedmon Mapana, ameipongeza taasisi ya Mama Ongea na Mwanao kwa juhudi zao za kugusa maisha ya watu wenye mahitaji maalum, hususan walemavu ambao wengi wao wamekuwa wakikutana na manyanyaso miongoni mwa wanajamii.

Ameongeza kuwa, kilichofanywa na taasisi hii ni cha kuigwa, pia, ni jambo la msingi watu au wadau kujitokeza kisha kusaidia watu wenye mahitaji maalum ili kuwatia moyo katika mapambano yao ya kila siku ya kutafuta riziki, hivyo ameisifu taasisi hiyo kwa kuwa mstari wa mbele kusaidia kundi hili lenye changamoto za kijamii.





Katibu Mtendaji ameenda mbali Zaidi baada ya kutangaza nafasi maalum kwa kundi la wasanii wa bendi ijulikanayo kama “Jumuishi Band,” linaloundwa na watu wenye mahitaji maalum, Bendi hiyo itapewa fursa ya kutumbuiza katika Tamasha la Muziki wa Dansi linalotarajiwa kufanyika Februari 2024, pamoja na kusajiliwa na BASATA bila malipo kama ishara ya kuwathamini.

## Wasanii waitikia wito wa “Rais” kupima afya zao






Na Isack N. Bilali

Katika hali ya kuhamasika zaidi ya wasanii 200 nchini wamejitokeza kuitikia wito wa kupima afya zao hususani moyo kwa ufadhili wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambaye ameendelea kuonesha namna anavyojali tasnia hiyo kwa kugharamia kampeni hiyo.

Akiongea wakati wa kutoa taarifa ya kampeni hiyo kwa wasanii, Katibu Mtendaji BASATA, Dkt. Mapana amesisitiza umuhimu wa kupima afya, ambapo kampeni ya kupima afya ya moyo kwa wasanii nchini imeanza mwezi Disemba, 2024 na itaendelea hadi Januari, 2025 ambapo kila wikiendi, wasanii watajumuika katika tawi la Kawe ili kuhakikisha wanapima afya zao kupitia wataalamu wabobezi katika sekta ya afya.

Ameendelea kusema kuwa, kampeni hii inafadhiliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambaye ametoa fedha kwa ajili ya kufanikisha zoezi hili kupitia Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), lengo ni kuhakikisha wasanii wanapata fursa ya kujua hali ya afya zao, hususan afya ya moyo, ambapo hadi kipindi cha Disemba, 2024 zaidi ya wasanii 200 tayari walikuwa wamejitokeza za kupima afya zao.





Akizungumza kwa niaba ya wadau wote, Dkt. Mapana ametoa shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Rais kwa mchango mkubwa na upendo wake kwa wasanii na Watanzania wote, amewataka wadau wa Sanaa na wasanii kuendelea kuitikia wito huo.






“Tunatoa wito kwa wasanii wote nchini kujitokeza kupima afya zao, Afya njema ni msingi wa mafanikio katika kazi na maisha kwa ujumla. Mungu aendelee kumbariki Mheshimiwa Rais na taifa letu kwa ujumla,” amesema Dkt. Mapana.





Pamoja na wasanii hao kufurika katika kampeni hiyo, viongozi, wadau mbalimbali wa Sanaa na wananchi wameoneshwa kuguswa na zoezi hilo lililojumuisha vipimo vya awali vya afya ya moyo, ushauri wa kitaalamu, na utoaji wa elimu kuhusu mbinu bora za kuishi maisha yenye afya, lilihudhuriwa na wananchi kutoka kada mbalimbali ambao walipata fursa ya kupima afya zao bure.



**Waziri mkuu atoa "sapoti" ya vifaa vya muziki kuinua Sanaa**

Na Isack N. Bilali

Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) linatoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mbunge wa Jimbo la Ruangwa, Kassim Majaliwa, kwa juhudi zake za kukuza na kuendeleza tasnia ya muziki nchini mara baada ya kukabidhi vifaa vya muziki kwa Bendi ya muziki ya Mkurupuko Jazz.

Mheshimiwa Majaliwa ametoa msaada wa vifaa vya muziki vyenye thamani ya shilingi milioni 20 kwa bendi ya muziki ya Mkurupuko Jazz, yenye maskani yake kijijini Mbekenyera, Wilaya ya Ruangwa, Mkoa wa Lindi akiwa ziarani, Mnamo tarehe 29 Disemba, 2024.

Tukio hilo limefanyika wakati wa mkutano wa hadhara uliofanyika katika kijiji cha Mbekenyera, ambapo Mheshimiwa Majaliwa alionesha dhamira yake ya kuunga mkono maendeleo ya sanaa kama sehemu ya kuchochea vipaji na kuimarisha ajira kwa vijana wa maeneo ya vijijini.

Msaada huu ni kielelezo cha uongozi wake imara wenye shauku ya kuona tasnia ya Sanaa hususani muziki inakua na kushamiri kuanzia ngazi za vijijini, kwakuwa imejidhihirisha kuwepo na vipaj lukuki vinavyohitaji kutiliwa mkazo kwa kuonesh wa njia ya kuibua.

BASATA inahimiza wadau wengine kuiga mfano huu wa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuhakikisha wasanii wanapata nyenzo na mazingira mazuri ya kuonyesha na kuendeleza vipaji vyao. Tunaamini kuwa msaada kama huu utachochea maendeleo ya sanaa ya muziki, kuimarisha uchumi wa wasanii, na pia kuhamasisha vijana kushiriki katika sanaa kwa bidii na ubunifu.

viongozi wa Mkurupuko Jazz wamefurahishwa na kutoa shukrani za pekee kwa Mheshimiwa mbunge wao kutokana na kutambua mchango wake mkubwa katika maendeleo ya sekta ya sanaa na kuimarisha utamaduni wa taifa ambap amewataka wanamuziki hao kuwa wabunifu ili vyombo hivyo viwe mtaji wa kukuza tasnia yao iwainue kiuchumi.



## “TRA na BASATA” zasomana kimifumo


Na Isack Bilali

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa kushirikiana na Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) wamesaini hati raasmi ya makubaliano katika ofisi kuu za TRA zilizopo Posta, jijini Dar es Salaam, tukio hilo limefanyika tarehe 24 Disemba, 2024 ikiwa ni hatua muhimu katika kuimarisha ushirikiano wa taasisi hizo mbili kwa lengo la kuboresha usimamizi wa kodi kwenye sekta ya sanaa nchini.

Katika hafla hiyo, Kamishna Mkuu wa TRA, Bw. Yusuph J. Mwenda, ametoa msisitizo wa umuhimu wa sekta ya sanaa katika uchumi wa nchi na kueleza hatua madhubuti zitakazochukuliwa kuhakikisha wasanii wanashiriki kikamilifu kwenye ulipaji wa kodi.

Amesema TRA itatoa elimu ya kodi kwa wasanii jambo ambalo litaasaidia kuwaelimisha wasanii kuhusu umuhimu na faida za kulipa kodi kwa maendeleo ya taifa na faida za kwao binafsi.



Ametoa pongezi kwa BASATA na wasanii kwa juhudi zao za kukuza sekta ya sanaa, hivyo Mamlaka ya Mapato ina jukumu la kuwasaidia wasanii katika mchakato wa ulipaji kodi, kupitia huduma za karibu na mifumo rahisi ya malipo kwakuwa wana nafasi kubwa ya kukuza mapato ya kwao na nchi.

"Wasanii wana nafasi kubwa katika kukuza mapato ya taifa kupitia sanaa wanazofanya, kwahiyo na inapendeza kuona wengi wao wamekuwa mfano bora kwa kulipa kodi kwa hiari."

Juu ya hapo, amewapongeza wasanii wote ambao wameweka kipaumbele katika ulipaji wa kodi, hatua inayochangia ongezeko la makusanyo ya mapato nchini, amewasihi kuendelea kufuatilia mabadiliko yanayofanywa na serikali ili iwe chachu ya maendeleo katika kazi zao.

Kwa upande wake, Katibu Mtendaji wa BASATA Dkt. Kedmon Mapana, amemshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiw Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa maono yake ya kuhakikisha mifumo yote ya serikali inafanya ka kwa ushirikiano.

"Rais wetu ametuwekea mazingira bora yanayowezesha sekta ya sanaa kushamiri kupitia mifumo inayosomana na inayolenga kutoa tija kwa kila mdau, hii ni hatua kubwa kwa sekta ya sanaa" amesema Dkt Mapana.

Amewapongeza wasanii na wadau wote wa sanaa kwa juhudi zao za kuendeleza sekta hiyo, ambapo amesisitiza kuwa makubaliano haya yataleta mabadiliko chanya katika ufanisi wa ulipaji kodi, uwazi, na maendeleo ya sekta ya sanaa nchini.












## "Magic vibe" watambua mchango wa Dkt Mapana katika sanaa




Na. Isack Bilali

Waandaaji wa Tunzo za "Magic vibe" wamemtunuku Katibu Mtendaji BASATA Dkt. Kedmon Mapana tunzo maalum ya heshima kutokana na juhudi anazofanya kuhakikisha sekta ya Sanaa inakuwa nchini

Tunzo hiyo maalum ya heshima imetolewa na waandaaji wa tarehe 15 Desemba, 2024 kama pongezi na kutambua mchango wake mkubwa katika kutengeneza mazingira ya kukuza na kuendeleza sekta ya sanaa.



Akizungumza baada ya kupokea tuzo hiyo, Dkt. Mapana aliwashukuru sana waandaaji wa Magic Vibes kwa kutambua juhudi zake. Aidha, ameielekeza tuzo hiyo kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, akimsifu kwa mchango wake mkubwa katika kuboresha mazingira na miundombinu kwa wasanii, hatua iliyosaidia kuipaisha sekta ya sanaa kimataifa.

Amesema kuwa, katika nyakati ambazo wasanii wanatakiwa kufanya kazi kwa bidii na ubunifu wote ni sasa kwakuwa wamebahatika kuwa na Rais anayejali sekta ya Sanaa kwa dhati kabisa, ndiyo maana leo hii kuna mazingira bora sana ya wasanii kufanya kazi zao.

"Tunahitaji kufanya maendeleo ya sanaa na sio kuwafungia wasanii, hii ni falsafa ambayo BASATA imeamua kwenda nayo ili kuhakikisha inaenda sambamba na matarajio ya Mheshimiwa Rais kwa kukuza na kuendeleza sekta ya Sanaa nchini" amesema Dkt Mapana.

Tuzo ya "Magic Vibes" ni moja ya matukio muhimu ambayo yanahusisha kutambua mchango wa wadau wa sanaa na burudani nchini, zinazotolewa kwa lengo la kuhamasisha ukuaji endelevu wa sekta hiyo.

## Wajumbe wa Bodi waungana na wasanii kupima afya ya Moyo

Na. Isack N. Bilali

Mwenyekiti wa Kamati ya maendeleo ya Sanaa BASATA Dkt. Gervas Kasiga, ameambatana na mjumbe wa kamati hiyo Bw. Single Mtambalike na Mkurugenzi msaidizi sehemu ya Sanaa za Maonesho Bi. Lilian Shayo ikiwa ni sehemu ya uhamasishaji wa kampeni ya kupima afya ya moyo kwa wasanii.

Zoezi la uhamasishaji wa upimaji wa magonjwa ya moyo limeendelea kushika kasi katika Hospitali ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), tawi la Kawe, lengo la kampeni hii ni kuongeza ufahamu na kuwahamasisha wasanii kuchukua hatua za mapema za kiafya ili kupunguza athari za magonjwa ya moyo.

Katika tukio hilo, Mwenyekiti wa Kamati ya maendeleo ya Sanaa Dkt. Gervas Kasiga, mjumbe wa kamati Bw. Single Mtambalike na Mkurugenzi msaidizi sehemu ya Sanaa za Maonesho BASATA, Bi. Lilian Shayo, walipata fursa ya kushiriki katika zoezi hilo na wasanii mbalimbali waliojitokeza, wakiwemo wanamuziki nguli, sarakasi, ufundi na wasanii wa filamu.

Wajumbe hao wa bodi, wakiongozwa na Mwenyekiti wa Kamati ya maendeleo ya Sanaa BASATA Dkt. Gervas Kasiga (Kaimu Katibu Mtendaji Bodi ya Filamu Tanzania) ametoa shukrani kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa moyo wake wa upendo kuhakikisha anafadhili kampeni hii ili wasanii waweze kupima afya ya moyo kupitia Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI).

Uhamasishaji huu unalenga kufanikisha upatikanaji wa huduma bora za afya na kuongeza ushirikiano kati ya taasisi za sanaa na afya kwa maendeleo ya jamii, hali hii inachochea wasanii wetu kuwa na tabia ya kuangalia afya zao mara kwa mara ili kuepuka madhara yanayoweza kuepukika.



## Katibu mkuu TAMISEMI ahimiza uharaka wa kuunganisha mfumo wa AMIS na TAUSI

Na Isack N. Bilali

Katibu Mkuu TAMISEMI ndugu Adolf H. Ndunguru amepongeza watumishi na uongozi wa BASATA na TAMISEMI kwa ushirikiano waliouanza katika kuhakikisha mifumo ya AMIS na TAUSI inaunganishwa na kusomana jambo ambalo litasaidia kurahisisha ufanisi wa utoaji huduma za kiuchumi kwa wananchi na Serikali.

Ameyasema hayo tarehe 05 Disemba, 2024 wakati akiaongea na watumishi na uongozi wa BASATA na TAMISEMI ambao wamekutana katika ukumbi wa Forest Sun set Mjini Morogoro ambapo amewataka kuongeza kasi ya ufanyaji kazi ili mifumo hiyo ianze kufanya kazi katika mwaka wa fedha 2024/2025 kama ilivyopangwa.

Ameendelea kusema kuwa suala la mifumo ya serikali kusomana siyo la hiyari bali ni maagizo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan wataalamu wamehimizwa kumaliza vipengele vilivyosalia ikiwemo suala la kisheria ili mifumo hii ikiungana yasainiwe makubaliano thabiti yatakayokuwa na uhalali wa kisheria hivyo kutoa faida kwa vizazi vya baadae nchini.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo Bw. Gerson Msigwa ametoa shukrani kwa Wizara ya TAMISEMI na wataalamu wake wakiongozwa na Katibu Mkuu wao kwa namna walivyolibeba jambo hilo kimkakati zaidi.

Ametoa wito kwa Baraza la Sanaa la Taifa kutumia ubunifu wa hali ya juu kuhakikisha wanatoa elimu ya kutosha kwa wadau wake ili waweze kuelewa faida ya matumizi ya mfumo.

Kikao hicho kimewakutanisha viongozi Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, BASATA na TAMISEMI ikiwa ni kikao kazi cha kupitia na kuona maendeleo ya uunganishaji wa mfumo wa TAUSI na AMIS katika ukumbi wa Forest Sun set Mjini Morogoro.








**Baadhi ya Watumishi wa BASATA wakiwa katika picha ya pamoja, mara baada ya kumaliza kikao cha kujadili uunganishaji wa mifumo ya TAUSI na AMIS mjini Morogoro**



**Mjumbe wa Bodi ya BASATA Dkt. Gervas Kasiga akikabidhi tuzo kwa Bwana Kim Kyando kutoka WASAFI, katika tukio la ugawaji wa tuzo za MAGIC VIBES zilizofanyika katika ukumbi wa the super dome-Masaki.**





**Wasanii wa kundi la WAMOTO kutoka Uswazi Born Talent wakifanya onyesho katika tamasha la filamu lililofanyika katika viwanja vya posta jijini Dar es salaam**

# PICHA KATIKA MATUKIO MBALIMBALI



**Baadhi ya Watumishi wa Baraza la Sanaa la Taifa katika picha za matukio mbalimbali**

# BODI YA UHARIRI

**Mwenyekiti**

Dkt. Kedmon Mapana

**Mkuu wa Kitengo**

Leonidas Tibanga

**Mwandishi**

Isack Bilal

**Msanifu**

Nicholaus Jofrey

8 Barabara ya Kivukoni,
Utumishi, Kitalu C,
S. L. P 4779,
DAR ES SALAAM.

Simu: +255 738 259 611/481,
Baruapepe: km@basata.go.tz
info@basata.go.tz

**Mfumo wa Wadau wa Sanaa,**
**Jisajili kupitia: https://sanaa.go.tz**

**www.basata.go.tz**

**basata.tanzania**